

HALMASHAURI YA WILAYA MWANGA

(Barua zote zilandikwe kupitia kwa Mkurugenzi Mtendaji)

MKOA WA KILIMANJARO

Simu Na: 027 2974343
: 027 2974344

E.Mail ded@mwangac.go.tz

Web site: www.mwangac.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. L.10/7/A/33



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
S.L.P. 176
MWANGA

13 Julai, 2021

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Mwangi imepokea kibali cha ajira mbadala chenye **kumb. Na. FA.170/370/01"B"/51** cha tarehe **14/06/2021** kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Raisi Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hivyo, natangaza nafasi za kazi kwa wataanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi ifuatayo:-

MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III – NAFASI 2

SIFA: Mwenye Elimu ya Kidato cha nne (IV) au sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo:-

Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii au Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na serikali.

MAJUKUMU.

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya Maendeleo ya Kijiji
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- v. Kutafisiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu
- vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika enco lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati au kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaaluma katika kijiji
- viii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za vijiji.


NGAZI YA MSHAHARA

Mshahara ni kwa mujibu wa viwango vya mishahara Serikali yaani TGS B.

MASHARTI YA JUMLA

1. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Mwanaga.
2. Mwombaji awe na umri unaoanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45 na awe na hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
3. Maombi yote, waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitokeza (Detailed C.V)
4. Maombi yote ya waombaji yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya elimu kidato cha IV au VI, cheti cha kuzaliwa na picha mbili za rangi za hivi karibuni (passport size) na iandikwe jina nyuma.
5. "testimonials, Provisional Results, Statement of Results" hati ya matokeo ya kidato cha nne au sita (FORM IV AND FORM VU RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.
6. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wakikishe vyeti vimchakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika TCU na NECTA na taarifa ya Uhakika iambatanishwe kwenye maombi.
7. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa UMMA hawataruhusiwa kuomba isipokuwa kama wanakibali cha **KATIBU MKUU** Kiongozi
8. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahasika watachukuliwa hatua za kisheria mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 27/07/2021 saa 9:30 alasiri
9. Taarifa nyingine muhimu tembelea tovuti ya Halmashauri www.mwangadc.go.tz
10. Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA,
S.L.P 176,
MWANGA.


Zefrin K. Lubuva
Mkurugenzi Mtendaji (W),
MWANGA.

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
YA MWANGA

Nakala: Katibu Mkuu,
Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya Ajira,
S.L.P 63100,
DAR ES SALAAM.